Kama unataka kujifunza zaidi njia ya Mkristo wa kweli anavyopaswa kuishi, basi ni lazima ujifunze Biblia. Ili kukusaidia; Kanise la Christadelphian Bible Mission limechapisha kijitabu kuhusu mafunzo ya Biblia kaitka somo hili muhimu.

Lina itwa Kuishi katika Ukweli. Unaweza kupata nakala kutoka Kanisa la Christadelphian, au kutoka anuani iliyoandikwa katika kijitabu hiki.

CBM Publishing
32 Blenheim Road, Far Cotton
Northampton, England. NN4 8NW

ISBN 1 902059 10 -7
Registered Charity Number: 248979 / 1020558
Company Number: 2796412

MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA YA WAKRISTADELPHIAN 28-31
Correspondence Course Lessons 28-31

MASOMO VA BIBLIA KWA NJIA VA POSTA YA WAKRISTADELPKIAN Na 28

MALAIKA

Soma: Waebrania 1

Malaika ni wajumbe wa Mungu. Wao wanaweza kuingia penye Utakatifu wa Mungu, hivyo wao inabidi wawe hawana dhambi. Hatuja ambiwa kuwa malaika wangapi, bali tunajuwa kuna idadi kubwa ya malaika. (Ona Waebrania 12:22; Mathayo 26:53.)

Malaika wanafanya nini?

- Kutoa ujumbe
- Kuongoza
- Kulinda na kuokowa
- Kuangamiza

Tuta tazama mifano kwa kugeuza kila moja ya haya hapo juu.

1. MIFANO YA MALAIKA WAKITOA UJUMBE

Neno "malaika" maana yake "mjumbe". Kuna mifano mingi ya wao wakitoa ujumbe wa Mungu kwa watu. Hapa kuna mifano michache:

ILIPO	MAELEZO
Mwanzo 18	Abrahamu aliambiwa kwamba yeye na Sara watapata mtoto. Malaika wameelezewa kuwa kama "watu", na kwa udhahiri walionekana hawa kutofautiana na watu wa kawaida. Mara nyingine malaika wanaweza kuonekana tofauti sana, hasa wanapo onyesha utukufu wa Mungu.
Mwanzo 19:1-5	Wakati ule malaika wawili walienda kwa Loti na kumuonya kwamba Mungu alikuwa anaenda kuuangamiza Sodoma. Watu wa Sodoma walifikiri kuwa malaika walikuwa ni wanadamu.
Mwanzo 22:11,15	Malaika alimwita Abrahamu toka mbinguni asimuue mwanawe, Isaka. Kisha malaika akambariki Abrahamu kwa imani yake na utii.
Kutoka 3:2	Musa aliambiwa kwamba Mungu atamtuma kwenda Misri ili kuwakombo a watu wa Israeli toka utumwani. Malaika a lye mpa ujumbe aliku wa katika kichaka kilichokuwa kinaungua na moto.

29D Ni uongo gani nyoka alio mwambia Eve katika Mwanzo sura ya 3?

30A Ibilisi ni nani?

30B Yesu aliziharibu vipi “kazi za ibilisi”?

30C Andika toka Mathayo 15:19. Kuhusu sisi wenyewe tunafundishwa nini?

30D Kwa nini tunahitaji kutubu?

31A Toa sababu nyingi unavyo weza ili kuonyesha kwa nini kumnyunyizia maji mtoto mdogo **sio** ubatizo unaosemwa na Biblia.

31B Kazi ya ziada
Ina maana gani Warumi 6:6?

31C Kazi ya ziada
Andika toka Wagalatia 3:27-29. Inatufundisha nini sisi?

Tuma majibu yako kwa:

Jina lako ni:

Christadelphian Bible Mission Box CBM, 404 Shaftmoor Lane,
Birmingham B28 8SZ, England

Waamuzi 6:11-24	Malaika alimwambia Gidioni kwamba Mungu atamsaidia kuwapiga maadui wa Waisraeli. Malaika alitokomea katika moto alio ufanya Gidioni.
Luka 1:11-19	Zakaria aliambiwa na malaika kwamba yeye na mke wake Elizabeti watakuwa na mtoto. Huyu alikuwa ni Yohana Mbatizaji.
Luka 1:26	Malaika Gabrieli alimwambia Mariamu atakuwa mama wa Yesu.
Matendo 8:26	Philipo aliambiwa akutane na towashi wa Ethiopia. Ndipo aliweza kumfundisha kuhusu Yesu na kumbatiza. (Angalia malaika ameitwa "roho" katika mstari wa 29.)

2. MIFANO YA MALAIKA WAKIONGOZA WATU

(i) Abrahamu alitaka mtumishi wake atafute mke kwa ajili ya Isaka mwanawe - lakini alikuwa awe ni mwanamke wa kufaa Abrahamu alimwambia mtumishi wake kwamba malaika atamsaidia (Mwanzo 24:7). Naye alifanikiwa!

(ii) Wakati Musa alipo waongoza watu wa Israeli toka Misri, nguzo ya wingu ilikwenda mbele yao. lliwalinda na kuwaongoza. Tuna ambiwa kwamba Malaika wa Mungu alikuwa pamoja nao katika nguzo wa wingu (Kutoka 14:19; Kutoka 23:20,21).

Ni muhimu kujua kwamba hata kama malaika wa Mungu alikuwa pamoja nao wakati wote hawa watu Israeli jangwani, bado walimuasi Mungu. Malaika hakuwazuia kufanya dhambi.

3. MIFANO YA MALAIKA WAKILINDA NA KUOKOWA WATU WA MU NGU

(i) Marafiki watatu wa Danieli waliokolewa na malaika kutoka kwenye tanuru ya moto (Danieli
3:27).

(ii) Danieli mwenyewe aliokolewa toka tundu Ia simba. Malaika alifunga vinywa vya simba (Danieli 6:22).

(iii) Malaika aliwafungua mitume toka gerezani (Matendo 5:19) na tena Petro (Matendo 12).

4. MIFANO YA MALAIKA WAKIANGAMIZA

(i) Wakati Yerusalemu ulipozungukwa na jeshi Ia waashuru katika kipindi cha Mfalme Hezekia, Hezekia aliomba msaada kwa Mungu. Malaika aliwaua Waashuru wote (ambao walithubutu kumshusha Mungu). Ona 2 Wafalme 19:35.

(ii) Mfalme Herodi, katika Agano Jipya nyakati zake, aliangamizwa na malaika kwa ajili ya kiburi chake kikubwa (Matendo 12:23).

Malaika hawafanyi dhambi

Katika wakati wa Kutoka, malaika walileta maangamizi yaliyo sababishwa na tauni. Kulielezea hill, mwandishi wa Zaburi anasema kwamba Mungu...

> *"…aliwatupia (Wamisri) ukali wa hasira yake, gadhabu na uchungu na taabu, kwa kuwatuma malaika wa mabaya kati yao" (Zaburi 78:49).*

Malaika wenyewe sio waovu, bali walitumiwa wa Mungu kufanya mambo tunayo yaona kama ya kutisha, lakini dhahiri yalikuwa ya lazima. Hakuna viumbe kama hawa malaika ambao wanatenda dhambi.

Lakini ni vipi kuhusu 2 Petro 2:4, ambayo inasema: Mungu hakuwaachilia malaika walio fanya dhambi ..." Neno lililofasiriwa "malaika" pia linaweza kutafsiriwa "wajumbe". Linaweza kuwa na maana wajumbe wa mbinguni (malaika), au wajumbe wa dunia (wanadamu ambao wanauchukuwa ujumbe).

MASWALI KARATASI YA 8

Jaribu na ujibu maswali katika maneno yako mwenyewe. Kwenye “kazi ya ziada” UNAWEZA kujibu au kuacha kama utaona maswali ni magumu. Tafadhali jaribu kujibu maswali mengine yote.

MOSOMO 28-31

28A Mafungu haya ya maneno yafuatayo yanatuambia nini kuhusu malaika?
- (a) Mathayo 26:53
- (b) Matendo 12:5-10
- (c) Waebrania 1:7
- (d) Luka 1:19

28B Kweli au si kweli?
- (a) Malaika wanaweza kutokea mbele ya Mungu.
- (b) Malaika wakati mwingine wanafanana na watu.
- (c) Malaika wengine wanafanya dhambi.
- (d) Malaika hawaowi.
- (e) Malaika hawazungumzi.
- (f) Malaika hawafi.
- (g) Malaika huwazuia waamini wasifanye dhambi.

29A (a) Mathayo 9:32-34 (b) Mathayo 12:22-45 (c) Mathayo 17:14-27
Watu katika mafungu haya ya maneno wameelezwa kama wana mashetani (mapepo). Katika dawa za kisasa leo tusinge wasema katika namna hii. Tungewasema wana matatizo gani?

29B Kwa nini Yesu alimwita Petro “Shetani”?

29C Watu wengine wanadhani shetani ni malaika ‘aliye anguka toka mbinguni (malaika ambaye amekuwa ni mwenye dhambi sana). Wazo hili unalifikiria vipi?

29D Ni uongo gani nyoka alio mwambia Eve katika Mwanzo sura ya 3?

30A Ibilisi ni nani?

30B Yesu aliziharibu vipi “kazi za ibilisi”?

30C Andika toka Mathayo 15:19. Kuhusu sisi wenyewe tunafundishwa nini?

30D Kwa nini tunahitaji kutubu?

31A Toa sababu nyingi unavyo weza ili kuonyesha kwa nini kumnyunyizia maji mtoto mdogo **sio** ubatizo unaosemwa na Biblia.

31B Kazi ya ziada
Ina maana gani Warumi 6:6?

31C Kazi ya ziada
Andika toka Wagalatia 3:27-29. Inatufundisha nini sisi?

Tuma majibu yako kwa:

Jina lako ni:

Christadelphian Bible Mission Box CBM, 404 Shaftmoor Lane,
Birmingham B28 8SZ, England

Lugha ya asili ambayo Biblia iliandikwa haiweki wazi Ikiwa ni wajumbe wa mbinguni au wa duniani wanao tajwa. Pengine walio tafsiri walikosea. Tunadokeza kwamba 2 Petro 2:4 inaweza vema kutaja kile kilicho andikwa katika Hesabu 16.



Malaika wanafananaje?

Aghalabu malaika wanafanya kazi zao pasipo kuonekana na watu. Wakati Elisha na watumishi wake walipokuwa wanawindwa na mfalme wa Syria, Elisha alijuwa Mungu atasaidia, lakini watumishi wake waliogopa. Elisha alimuomba Mungu afunue macho ya watumishi wake. Ndipo aliona...

> "…mlima ulikuwa na farasi tele na magari ya moto kumzunguka pande zote Elisha" (2 Wafalme 6:17).

Jeshi la Mungu Ia malaika lilikuwepo pale kulinda!

Tayari tumekwisha ona kwamba malaika walio mtokea Abrahamu na Loti walifanana na wanadamu (kwa hiyo hawakuwa na mabawa!) bali tumeona pia malaika waliweza kuwa katika moto na wingu, kama katika kichaka kilichokuwa kinaungua na nguzo ya wingu jangwani. Hivyo malaika hawana umbo lolote la kitu kimoja na anaweza kutoweka tu (kama mmoja alivyo fanya kwa Gibioni alipo mtembelea).

Yesu na malaika

Malaika waliwaambia Yusufu, Mariamu na wachungaji wa wanyama kuhusu kuzaliwa Yesu. Waliendelea kumuongoza Yusufu kwa kumwambia amchukue mtoto Yesu watelemke kwenda Misri na kisha ilipokuwa salama wakati wa kurudi.

Zaburi 91 (mstari 11) ilitabiriwa kuwa malaika watamsaidia Yesu na hivyo, kwa mfano, katika Mathayo 4:11 tunasoma kwamba baada ya majaribu yake jangwani, malaika "walifika na kumtumikia". "Kutumika" ni "kuhudumia" na ndipo ni kama kwamba malaika walimletea chakula baada ya funga ya muda mrefu.

Katika bustani ya Gethsemani, wakati Yesu alipojuwa kusulubiwa kwake kumkaribia, aliomba ili afanye mapenzi ya Mungu. Malaika walimtia nguvu (Luka 22:43). Angeweza kuepuka kukamatwa na angemuomba Mungu amtumie askari kumi na mbili wa malaika wamuokoe asikamatwe. Lakini alijuwa kwamba ilimpasa afe kwa ajili yetu. Ilikuwa ni njia pekee ya kutuwezesha sisi kutoka katika hali yetu ya dhambi.

Tungetegemea Mungu angemfanya Mwanae kuwa kama malaika, bali alikuwa ni mwanadamu. Katika umbo Ia kibinadamu tu aliweza kupata majaribu, kuteseka na kisha kufa. Malaika hawafi (Luka 20:36).

Waebrania 2:9 inasema kwamba Yesu "alifanywa kuwa mdogo kuliko malaika kwa mateso ya mauti" (ona pia Waebrania 2:16).

Alipo fufuka toka wafu malaika walikuwepo pale. Fifiria furaha yao! Kushinda dhambi na mauti, Yesu aliinuliwa akawa juu ya malaika. Hana mwili wa mwanadamu tena:

> *"Wakati yeye (Yesu) mwenyewe alipo fanya utakaso wa dhambi zetu, aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu; amefanyika bora kupita malaika..." (Waebrania. 1:3,4)*

MASWALI KARATASI YA 8

Jaribu na ujibu maswali katika maneno yako mwenyewe. Kwenye “kazi ya ziada” UNAWEZA kujibu au kuacha kama utaona maswali ni magumu. Tafadhali jaribu kujibu maswali mengine yote.

MOSOMO 28-31

28A Mafungu haya ya maneno yafuatayo yanatuambia nini kuhusu malaika?
- (e) Mathayo 26:53
- (f) Matendo 12:5-10
- (g) Waebrania 1:7
- (h) Luka 1:19

28B Kweli au si kweli?
- (h) Malaika wanaweza kutokea mbele ya Mungu.
- (i) Malaika wakati mwingine wanafanana na watu.
- (j) Malaika wengine wanafanya dhambi.
- (k) Malaika hawaowi.
- (l) Malaika hawazungumzi.
- (m) Malaika hawafi.
- (n) Malaika huwazuia waamini wasifanye dhambi.

29A (a) Mathayo 9:32-34 (b) Mathayo 12:22-45 (c) Mathayo 17:14-27
Watu katika mafungu haya ya maneno wameelezwa kama wana mashetani (mapepo). Katika dawa za kisasa leo tusinge wasema katika namna hii. Tungewasema wana matatizo gani?

29B Kwa nini Yesu alimwita Petro “Shetani”?

29C Watu wengine wanadhani shetani ni malaika ‘aliye anguka toka mbinguni (malaika ambaye amekuwa ni mwenye dhambi sana). Wazo hili unalifikiria vipi?

4. Tukibatizwa, tuna anza maisha mapya “katika Kristo” (tazama Warumi 6:3,4).

Sura za kusoma: Soma tena habari katika Matendo 8,9 na 10.
Pia Warumi 6
Mstari wa kujifunza: Warumi 6:3,4

> *“Hamufahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake: kusudi kama Kristo alivyo fufuka toka wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzime.”*

Heshima ya kuketi mkono wa kuume wa Mungu ni kwa ajili ya Yesu peke yake, namna hii hakuna malaika aliye wahi kubahatika (Waebrania 1:13). Badala yake katika sura hii hii malaika wameelezwa (katika mstari 7) kama "roho na watumishi wake mwali wa moto". Mstari wa 14 unasema:

> "Je! hao (malaika) wote sio roho watumikao, wakitumwa kuwahudumu wale watakao urithi wokovu?"

(Angalia neno **"wote"** - hakuna nafasi ya malaika hapa wanaofanya dhambi.)

Malaika wanafanya kazi kwa niaba ya wale ambao watarithi wokovu. Tumeona kwenye suala Ia towashi wa Ethiopia jinsi malaika alivyo mleta mahali alipo weza kujifunza ukweli wa Injili. Tumeona mitume walivyo saidiwa kutoka gerezani. Lakini malaika hawamsaidii kila mtu! Wanahudumu kwa wale "ambao watarithi wokovu" (Waebrania 1:14).

Kazi ya malaika leo

Hata kama hatuwaoni, malaika wanaweza kutusaidia leo, akin kama tukijaribu tu kumpendeza Mungu. Zaburi 34:7 inasema kwamba malaika wanawazunguka **wale ambao wanamcha Yeye.** Wanaweza kutusaidia akin hii haina maana kusema kwamba waamini kamwe hawatakuwa na nyakati ngumu. Nyakati ngumu katika maisha zipo ili kutufundisha mambo ya kujifunza na kutuleta karibu ya Mungu. Aidha malaika hawawezi kuwazuia waamini wasifanye dhambi. (kumbuka jinsi malaika katika jangwa hakuweza kuwakomesha watu wa Israeli kutokufanya dhambi).

Kazi ya baadaye ya malaika

Bwana Yesu Kristo sio muda mrefu atarudi duniani, lakini hakuna hata mmoja anaye juwa ni lini, hata malaika wa Mungu mbinguni (Marko 13:32). Wakati atakapo kuja, malaika watakuja pamoja naye. 2 Wathesalonike 1:7,8 wasema:

"Bwana Yesu atafunuliwa toka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake, katika mwali wa moto kuja kuwalipiza kisasi wale wasio mjuwa Mungu, na wale wasio itii Injili ya Bwana wetu Yesu Kristo....

Malaika watahusika katika kuwakusanya pamoja watu kwa ajili ya hukumu.

Wakati huo, waamini watafanywa kuwa kama malaika. Hawata owa tena, au kufanya dhambi, au kufa (Angalia Mathayo 22:30; Luka 20:36). Sio ajabu kuna furaha mbinguni (katikati ya malaika) wakati mwenye dhambi anapotubu!

Muhutasari

1. Malaika ni wajumbe. Pia wanaweza kuongoza, kulinda, kuokowa na kuangamiza.
2. Wawasaidia wale ambao ni waamini wa kweli, lakini hawawazui watu kufanya dhambi.
3. Aghalabu hawaonekani. Wakati walipo onekana walitokea katika namna nyingi tofauti.
4. Hawatendi dhambi, hawaowi, na kamwe hawafi. Katika Ufalme, waamini watakuwa kama hivi.
5. Mara ya kwanza Yesu alifanywa punde kuwa mdogo kuliko malaika, lakini baada ya ufufuo alipandishwa kuwa juu yao.
6. Malaika watamfuata Yesu wakati atakapo kuja duniani.

Sura za kusoma:

Tazama mafungu yaliyotolewa katika somo. Soma tena yote mpaka ufahamu vema malaika kazi yao wanayo ifanya kwa ajili ya Mungu.

Mstari wa kujifunza: Waebrania 1:14

"Je hao wote sio roho watumikao, wakitumwa kuwahudumu wale watakao rithi wokovu?"

Akamwambia Nikodemo:

"Mtu asipo zaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia Ufalme wa Mungu" (Yohana 3:5).

Kumbuka maneno tuliyo anza nayo – "Aaminiye na kubatizwa ataokoka; bali asiye amini atahukumiwa." Watu wote ni wenye dhambi, dhambi huleta mauti. Kifo ni mwisho wa uhai, na hakuna cha kutumainia baadaye. Hakuna tumaini – ila tuzaliwe tena na tubatizwe.

Maisha Mapya

Kuamua kubatizwa ni uamuzi wa muhimu zaidi mtu yeyote anaweza kufanya. Sio uamuzi wa kuuchukuwa kirahisi.

Kabla ya ubatizo - yatupasa tufahamu na tuamini mafundisho ya kweli ya Biblia.

Baada ya ubatizo - inatubidi tufanye vita juu ya dhambi zetu, na tumtumikie na tujaribu kutii maagizo ya Mungu.

Tunaweza kutimiza hili kama tukisoma Neno Lake. Itatubidi tuache kutenda mambo yasio mpendeza Mungu. Hii itakuwa na maana tutatumia muda mchache kuwa pamoja na watu wasio jishughulisha na Mungu, hata kama walikuwa ni marafiki zetu, kwa sababu wanaweza kutupeleka mbali toka kwa Mungu. Itakuwa ni bidii ya kila siku, lakini italeta thawabu nyingi. Yesu aliwahi kusema:

"Na kila mtu aliye acha nyumba, au ndugu wa kiume, au wakike, au baba au mama, au mke, au watoto, au mashamba, kwa ajili ya jina langu atapokea mara mia, na kurithi uzima wa milele" (Mathayo 19:29).

Muhutasari

5. Mungu ametuagiza tubatizwe.
6. Ubatizo ni kuzikwa kabisa ndani ya maji.
7. Katika mfano, tunakufa pamoja na Kristo na kutoka kwenye maji kuelekea maisha mapya.

Ujumbe ni –

- Watu inawapasa kwanza wasikie ujumbe wa injili.
- Inawapasa waamini kwa moyo wao wote.
- Inawapasa waiache njia yao wenyewe nao waelekee njia za Mungu.
- Kisha inawapasa wabatizwe.
- Na hivyo wana anza maisha mapya katika Kristo.

Maana ya ubatizo

"Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake: kusudi kama Kristo alivyo fufuliwa toke wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi pia tuenende katika upya wa uzima" (Warumi 6:4).	Bwana Yesu alisulubiwa. Mwili wake ulio kufa ulilazwa kaburi ni. Baada ya siku tatu, Mungu alimleta uzimani tena.

Tukifahamu kwamba Bwana aliteseka na alikufa kwa ajili yetu, tutasema kama Wayahudi siku ya Pentekosti, "Tutafanyaje?" Jibu ni lile lile leo:

"Tubuni, na mbatizwe".

Maana ya kweli ya ubatizo ni nini?

Kama mwili wa Yesu ulivyo zikwa kaburini, basi katika ubatizo mwili wetu unazikwa katika maji. Tume "zikwa pamoja naye". Kwa njia hii, tuna kiri kwamba tunastahili kufa kwa sababu ya dhambi zetu. Kuzikwa katika maji, ni kuonyesha kwa mfano, kufa pamoja na Kristo. Na kama alivyo toka kaburini, vivyo hivyo tunatoka majini. Huku ni kuzaliwa tena, na maisha mapya yana anza.

Kuzaliwa mara ya pili

Myahudi aliye itwa Nikodemo alimjia Yesu usiku na kumuuliza kuhusu mafundisho yake (Yohana 3). Yesu akamwambia, "Yakupasa uzaliwe mara ya pili". Nikodemo aliona hiyo haiwezekani – na, kwa kweli ndivyo ilivyo, ukiyachukuwa maneno ya Yesu bila kufahamu maana yake. Lakini Yesu alikuwa anasema kuzaliwa upya kwa ubatizo.

MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA YA WAKRISTADELPHIAN Na 29.

MASHETANI (MAPEPO), NA SHETANI

Soma: Mathayo 8:14-34

MASHETANI NA MAPEPO

Kuna maneno mawili ya Kiyunani ambayo yametafsiriwa "ibilisi" katika Biblia zetu, na kama yana maana ya vitu tofauti, kwa kweli tunahitaji kujuwa maana ya kila neno. Nayo ni:

daimon - ambalo maana yake ni "roho mchafu"
diabolos - ambalo maana yake ni "singizia au congea"

Tutaona neno ibilisi (diabolos) kwenye somo lifuatalo.

Neno daimon. limetumika katika lugha ya Kiyunani tunapo ambiwa kwamba "Yesu alikemea au alitoa mapepo". Yesu aliponya kila aina ya magonjwa ambayo watu wanauguwa. Vipofu aliwafanya waone; viziwi walisikia; vilema walitembea. Pia aliwaponya watu walio kuwa wanateswa na magonjwa ya akili, na wenye huzuni kama kifafa.

Katika siku hizo, wakati magonjwa yalipokuwa vigumu kuyatambua, watu walisema kwamba mwenye kuuguwa alikuwa "ameshikwa na pepo". Yesu alipowaponya watu kama hawa, alisemwa kuwa "ametoa pepo".

Soma kwa makini Mathayo 8:16-17. Tuna ambiwa kwamba

"…watu walimletea wengi walio shikwa na mashetani (mapepo): aliwatoa roho kwa neno lake, na aliwapomya wote walio kuwa hawawezi."	Yesu alisema kwamba Isaya alitabiri kuhusu hili alipo seme:	"Yeye mwenyewe aliutwaa udhaifu wetu na alichukuwa magonjwa yetu" (Isaya 53:4)

Hii inatuonyesha kwamba

"ibilisi au kushikwa na pepo"	Ni mamoja	"udhaifu" au magonjwa

Sanamu zilizo kuwa "mashetani"

Katika sehemu zingine katika Biblia ambazo neno daimon limetumika, mara nyingi zinataja kuabudu sanamu. Geukia kwenye Zaburi 106. Zaburi hii inatuambia yote ambayo maovu Wa-Israeli waliyatenda, na jinsi, ingawa walifanya yote hayo, Mungu aliendelea kuwabariki. Soma mistari 35-38. ambayo mwandishi wa Zaburi anawasema wa-Israeli:

> *"Walizitumikia sanamu zao: ambazo zilikuwa mtego kwao. Naam. walitoa wana wao na binti zao kuwa sadaka kwa mashetani."*

Neno "mashetani" hapa katika Agano la Kale ni sawa na daimon au pepo. Katika mstari 37 lawama zimerudiwa. lakini muda huu tumeambiwa kwamba "walitoa wana wao wawe dhabihu kwa **sanamu**". Kwa udhahiri. wakati ule. "mashetani" waliotajwa hapa walikuwa ni masanamu ya mataifa yalio izunguka Israeli.

Kuna mfano mmoja wa kutumia neno katika Agano Jipya, katika 1 Wakorintho 10:20. Paulo anawaambia Wakorintho kuwa watu wa mataifa "wanatoa dhabihu kwa mashetani, na sio kwa Mungu". Kama ukiangalia nyuma kwenye mstari wa 19, utaona kwamba hawa "mapepo" kwa kweli walikuwa ni masanamu.

Wakristo walimwabudu Mungu mmoja wa kweli; miungu mingine yote walikuwa ni masanamu, hapa wameitwa "mashetani"; vitu visivyo na uhai ambavyo watu waliviabudu bure.

Angalia: neno linalo maanisha "roho mchafu" (daimon) mara kwa mara limetafsiriwa **mashetani** katika Biblia za A.V. na lisichanganyishwe na ibilisi. Tafsiri zingine mara nyingi zina mapepo badala ya mashetani.

SHETANI

Shetani katika Agano la Kale maana yake ni "adui" au "anaye pinga".

1 Wafalme 11:14 chasema: *"Na Bwana alimsimamishia Sulemani adui Hadadi Mwedomi."*

11:23 chasema: *"Naye Mungu alimsimamishia adui mwingine, Rezoni mwana* wa *Eliada...*

11:25 unaongeza: *"Alikuwa adui kwa Israeli siku zote za Sulemani"*

Ndipo wote wawili **wakatelemka majini** (hivyo halikuweza kuwa ni jambo la kumnyunyizia). Basi Philipo akambatiza yule towashi. Baada ya hili, tumeambiwa kwamba walipo toka majini Philipo alihamishwa na Mwethiopia alikwenda njia yake akifurahi. Aliipata njia ya uzima.

Habari ya akida wa Kirumi

Soma habari hii katika Matendo 10. Kornelio akida alikuwa "mtu mtauwa, anaye mcha Mungu, yeye na nyumba yake yote, naye alikuwa akiwapa watu sadaka nyingi, na kumwomba Mungu daima". Unaweza kufikiri kulikuwa hakuna chochote zaidi cha kuweza kufanya.

Lakini kulikuwa na kitu kingine zaidi cha kufanya. Mungu alimtuma malaika kwa Kornelio na malaika alimwambia atume watu wakamwite mtume Petro. Malaika akasema, "Yeye atakuambia yakupasayo kutenda".

Sasa Petro, akiwa Myahudi, asingekwenda kamwe kwenye nyumba ya mtu wa mataifa (yaani mtu asiye Myahudi). Lakini Mungu alizungumza naye katika njozi, na aliambiwa kwenda na watu walio tumwa na Kornelio. Mpaka muda huo, ni Wayahudi tu waliokuwa wame itwa na Injili.

Petro alipo fika kwenye nyumba ya Kornelio, alimkuta akida akimsubiri pamoja na jamaa na rafiki zake. Alimkaribisha Petro, na akamweleza kuhusu malaika aliye mtembelea. "Sasa basi", akasema, "sisi sote tupo hapa mbele za Mungu, tupate kusikia maneno yote uliyo amriwa na Mungu" (mstari 33). Petro akawaambia watu pale kuhusu Yesu; uzima wake na kifo na ufufuo. Kabla hajamaliza kusema, zawadi maalum ya Roho Mtakatifu iliyokuwa imetolewa kwa waongofu wa Kiyahudi ikawashukia wale walio kuwa wanasikiliza. Hakuna mtu aliweza kuwa na shaka wakati ule maana Mungu aliwakubali. Basi hatua ya muhimu ilichukuliwa. Petro akasema:

> *"Ni nani awezaye kukataza maji, hawa wasibatizwe, watu walio pokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi? Akaamuru wabatizwe kwa jina lake Yesu Kristo" (mistari 47-48).*

Somo lipo dhahiri – lisilo badilika zuri la kuonyesha kweli, wacha-Mungu wanaweza tu kuwa washirika wa Kanisa la Kristo wakibatizwa.

Alipo ona jinsi alivyo kosa, alikuwa tayari kutoa maisha yake yaliyo bakia ili amfuate Yesu. Yesu alimtuma mwanafunzi wake aliye itwa Anania kwake, na Anania alimsaidia ili apate kuona tena, na alimwambia abatizwe (ona Matendo 9:17-18). Basi Paulo alipo amini ukweli kuhusu Yesu, alizisikitikia njia zake za awali, naye alianza maisha mapya alipo batizwa.

Kuna maelezo mengi katika Matendo ya Mitume ya watu walio amini, wali igeukia njia ya Mungu nao walibatizwa.

Masimulizi yanayo muhusu towashi wa Ethiopia

Soma katika Matendo 8:26-40. Towashi alikuwa ni wamuhimu serikalini. Alikuwa Yerusalem u ili kumwabudu Mungu. Alipokuwa anasafiri kurudi nyumbani, alikuwa anasoma Isaya 53, inayosimuliwa mateso na kifo cha Masihi. Hakufahamu wakati alipokuwa anasoma–



“Aliongozwa kwenda machinjoni kama kondoo; na kama vile mwana-kondoo alivyo kimya mbele yake amkataye manyoya, vivyo hivyo yeye naye hafunui kinywa chake: katika kufedheheshwa kwake hukumu yake iliondolewa, ni nani atakaye yaeleza kizazi chake? maana uzima wake umeondolewa katika”
(Matendo 8:32-33)

Mara aliungana na mfuasi aliyeitwa Philipo, ambaye alitumwa na Mungu ili amsaidie. Philipo alimuuliza iwapo aliyafahamu aliyo kuwa anayasoma, towashi alijibu, “Nitawezaje kuelewa, mtu asiponiongoza?” Basi Philipo akamweleza fungu la maneno na kumhubiria kuhusu Yesu. Halafu baadaye wakafika kwenye maji, naye towashi akasema:

“Tazama, maji haya; ni nini kinachonizuia nisibatizwe?”

Angalia jibu kwa makini. Philip akasema

“Ukiamini kwa moyo wako wote, inawezekana.”

Sulemani alianza vema akiwa mfalme na alimpenda Mungu, na kisha akaja kuingia kwenye ibada ya sanamu, ndipo Mungu alimpelekea maadui. Neno hili "adui" katika I Wafalme 11 ni neno halisi lililo sawasawa na "shetani" kama lilivyo tafsiriwa mahali popote. Hadadi na Rezoni walimletea Sulemani matata na Israeli, nao "walimpinga" Sulemani na Israeli kwa ujumla sababu walikuwa wanafanya dhambi. Walikuwa ni "shetani" kwa Sulemani na Israeli.

Shetani siku zote siye adui mbaya. Katika Hesabu 22:22 tumeambiwa habari za nabii aliyeitwa Balaamu, alikuwa anakwenda njia ambayo Mungu hakuitaka afanye. Habari inasema:

> *"Mungu hasira yake ikawaka kwasababu alikwenda; na malaike we Bwana alisimama kwenye njia akiwa adui juu yake"*

Ni dhahiri neno haliwezi kuwa na maana ya kiumbe muovu. Maana neno "adui" katika Agano la Kale hapa pia ni "shetani"; basi hapa tuna malaika wa Mungu mwaminifu, akifanya mapenzi ya Mungu, naye ameitwa "shetani". Kwa hiyo "shetani" ni adui, aliye katika upinzani. Anaweza kuwa mwema au mbaya.

SHETANI MAANA YAKE NI ADUI AU MTU ANAYE PINGA

Wakati Petro alipojaribu kumgeuza Yesu toka kwenye njia ambayo Mungu alimtaka aende, akawa adui, na Yesu alimwambia: *"Rudi nyuma yangu Shetani"* (Mathayo 16:23). Kwasababu alikuwa anajaribu kumgeuza kutoka katika njia ya Mungu, Petro akawa "shetani" maana alikuwa anampinga Yesu.

Basi shetani katika Agano Jipya pie maana yake ni adui. Adui mkubwa wa mwanadamu ni nafsi yake mwenyewe ye dhambi na hivyo neno "shetani" linaweza kutumika kwa maana hii. Hii inaweza kuonekana kwa kulinganisha Matendo 5 mistari 3 na 4:

MSTARI 3: "Petro akamwambia Anania, kwanini Shetani ameujaza moyo wako hate ukamdanganya Roho Mtakatifu..."	MSTARI 4: "Kwa nini umeliweka jambo hili moyoni mwako? Huku mdanganya mwanadamu bali Mungu."

Ilikuwa ni mawazo ye dhambi yake mwenyewe Anania. "Shetani" ametumika katika mstari wa 3 kuwa badala ya hali ya dhambi ya Anania, ambayo ilikuwa inapinga mambo ya Mungu.

Lusifa alikuwa ni nani?

lsaya 14:12-16 mara nyingi watu wameinukuu ambao wana amini kuwa yupo kiumbe muovu asiye wa kawaida:

> *"Jinsi ulivyo anguka toka mbinguni, Ee Lusifa, mwana wa alfajiri! jinsi ulivyo katwa kabisa hadi chini ewe uliye waangusha mataife...*

Ni dhahiri kabisa, kama ukisoma sura nzima utaona kwamba Lusifa na mfalme we Babeli (angalia hasa mstari wa 4). Ulikuwa ni unabii wa kuanguka kutoka kwenye mamlaka mfalme wa Babeli.

Katika njia ileile Ezekieli 28:14-16 wakati mwingine imedhaniwa kuwa inataja kiumbe muovu kupita kawaida:

> *"Wewe ulikuwa kerubi mwenye kutiwa mafuta afunikaye; nami nalikuweka wewe hivyo: ulikuwa juu ye mume mtakatifu wa Mungu... ulikuwa mkamilifu siku zako zote … hata uovu ulipo kutwa kwako."*

Ni wazi kwamba sura hii inamtaja mfalme wa Tiro, kama katika mstari wa 12 unavyo onyesha, nao hauna chochote cha kumtaja kiumbe aliye zaidi kupita wote.

Kulitokea nini katika Bustani ya Edeni?

Je, unakumbuka kilichotokea kwenye Bustani ya Edeni? Wakati Mungu alipo mwita Adamu toke mafichoni na alipo muuliza iwapo alikula matunda ya Mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya, Adamu alijibu:

> *"Mwanamke ambaye **wewe** umenipa awe pamoja nami, **amenipa** nami nikala."*

‘Kubatiza’ watoto wadogo kwa kuwanyunyizia maji hakuja fundishwa katika Biblia

Tumefundishwa wazi kabisa kuwa imani ije kabla ya kubatizwa. Mtoto awezaje kuamini kabla hajawa mkubwa vya kutosha ili afahamu?

Wayunani walitumia neno ‘kubatiza’ walipokuwa wanabadili nguo rangi. Nguo ‘ilibatizwa au waliitosa ndani ya maji. Hakuna sehemu ya nguo iliyoweza kuachwa nje ya maji ya rangi, au kuibadili kungekuwa na mabaka mabaka. Kwa njia hiyo hiyo wakati Biblia inapozungumzia ubatizo, inamaanisha kutosa kabisa ndani ya maji. Kuna maana nzuri kwenye tendo hili la kuzikwa ndani ya maji, na kisha kutoka tena, kama tutakavyo ona baadaye.

“Tubuni na mbatizwe”

Tayari kama tulivyo kwisha ona, huu ulikuwa ni ujumbe wa Yohana Mbatizaji. Injili ina waita watu wabadili mawazo yao na njia zao, nao wamrudie Mungu. Hii ndiyo maana ya Biblia inapo isema ‘toba’.

Petro alitoa ujumbe ule ule kwa Wayahudi siku ya Pentekosti. Walikuwa wamekwenda njia mbaya; hawakutambua kwamba Yesu wa Nazareti alikuwa ni Mwana wa Mungu, aliye tumwa kwao. Walihusika na kifo chake. Walipo tambua walicho fanya, waliwaambia mitume, “Wanaume na ndugu, tufanye nini?” Unaweza kusoma jibu la Petro katika Matendo 2:38:

> *“Kisha Petro akawaambia, Tubuni, na mbatizwe kila mmoja wenu katika jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi.”*

Ubatizo wa mtume Paulo

Mtume Paulo ni mfano mzuri wa njia ya toba inayo ongoza kwenye ubatizo. Paulo alikuwa anakwenda njia mbaya. Alikuwa anawatesa wafuasi wa Yesu; hakika hakuamini kuwa Yesu alikuwa ni Mwana wa Mungu. Alipokuwa ana safiri kuelekea Dameski ili kuwatesa Wakristo kule, Bwana alimtokea na kuzungumza naye. Paulo alipomuona Yesu, ilibidi afikiri tena. Hatimaye alimtambua Yesu kwa kweli alikuwa ni nani.

Baada ya kufufuka toka kaburini, na kabla tu hajapaa kwenda mbinguni, Bwana Yesu aliwaambia mitume wake:

> *“Enendeni duniani pote, na mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; lakini asiye amini atahukumiwa” (Marko 16:15-16).*

Mambo mawili yapo wazi sana toka maneno haya.

1. Kabla mtu yeyote hajaweza kuamini na kubatizwa, inabidi aijuwe injili iliyofundishwa na Yesu, na afahamu habari njema za Ufalme wa Mungu.
2. Kuhusu ubatizo hakuna awezaye kujifurahisha – sio kitu kingine ambacho tunaweza kufanya iwapo tunaona tunapenda. Ni wa muhimu. Mtu asipo amini na kubatizwa ajue amehukumiwa mauti, na hana tumaini la uzima ujao.

Toba huja kabla ya ubatizo

Wakati mtu anapo isikia Injili na anaielewa, inabadilisha fikira zake. Ana anza kugeuka toka njia yake kuelekea njia ya Mungu. Ubatizo ni njia aliyo tuchagulia Mungu ili kuanza upya. Wakati tunapo mgeukia Yeye, na tunapo tii agizo Lake la kubatizwa, dhambi zetu zinasamehewa, nasi tunaweza kuanza maisha mapya.

Yesu ametupa mfano

Kamwe Yesu hakufanya kitu chochote kibaya. Hakuwa na haja ya kubatizwa ili kwamba dhambi zake zisamehewe, kwa sababu kamwe hakutenda dhambi. Katika Mathayo 3:13-17 unaweza kusoma jinsi Yesu alivyo shuka chini kwenye mto Yordani, na alivyo batizwa katika mto na binamu yake Yohana. Yohana alijuwa Yesu hakuwa na dhambi kamwe, naye alimwambia hastahili kumbatiza. Hii ilikuwa ni kweli; lakini Yesu alimwambia:

> *“Kubali hivi sasa: kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote” (Mathayo 3:15).*

Kwa kubatizwa kwake, Yesu ametuwekea mfano wa kuufuata.

Tuna maana gani kwa Ubatizo?

Umeliona fungu la maneno katika Mathayo, Yesu alibatizwa pale Yordani, na halafu “alitoka mara hiyo nje ye maji”?

Kwa kweli Adamu alikuwa anajaribu kusema kwamba lawama zimpate Mungu kwa kumpa mwanamke, na laumu impate mwanamke kwa kumpa tunda. Lakini kosa **lilikuwa** ni **lake mwenyewe.**

Kisha Mungu alimuuliza mwanamke nini alilo lifanya, naye alisema:

> *"Nyoka alinidanganya, nami nikala"*

- katika maneno mengine, mwanamke alimlaumu nyoka; lilikuwa ni kosa la nyoka.

Adamu na Eva walikuwa na mashaka ya kumlaumu mwingine zaidi, kuliko kuichukuwa lawama kwa matendo yao maovu. Sisi sote tupo namna hiyo. Hatupendi kuhusika na matendo yetu wala mawazo mabaya tunayo yafanya. Pengine hiyo ndiyo sababu wetu wengi wanaamini kwamba kuna kiumbe-anyepita wanadamu anaye itwa "ibilisi" ambaye anawashawishi kutenda dhambi wanaume na wanawake.

Mungu aliruhusu nyoka anene, kiasi kama alivyo ruhusu punda wa Balaamu kusema (Hesabu 22:28). Adamu angeweza kuongoza na kumchunga nyoka katika sehemu yake, lakini sasa Mungu aliruhusu Adamu na Eva wajaribiwe - nao walishindwa. Nyoka **hakuwafanya** wao wale tunda, nyoka alitoa jaribu tu. Adamu na Eva waliamua wao wenyewe kula matunda.

Muhutasari

1. Mapepo yaliyo tolewa na Yesu yalikuwa ni magonjwa yaliyo dhaniwa kuwa yalisababishwa na roho wachafu walio washika watu kwa maradhi fulani.
2. Neno mashetani au mapepo ni tofauti na neno ibilisi (ambalo litaonwa kwenye somo litakalo fuata).
3. "Shetani" maana yake ni adui - mtu anaye pinga. Adui anaweza kuwa mwema au mbaya,
4. Lusifa katika lsaya 14 anatajwa mfalme wa Babeli, sio kiumbe anayepita kawaida.

Sura za kusoma: Mathayo 16:21-28; Hesabu 22
Mistari ya kujifunza: Mathayo 8:16-17

"Hata ilipofika jioni walimletea wengi walio pagawa na pepo: naye alitoa roho kwa neno lake, aliwaponya wote waliokuwa wagonjwa: ili litimie lililo nenwa na lsaya nabii kusema, Yeye mwenyewe aliiutwaa udhaifu wetu na alichukuwa magonjwa yetu".

MASOMA YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA YA WAKRISTADELPHIAN

Na30.

IBILISI NA DHAMBI

Somo: Waebrania 2:9-18

Bila shaka Biblia inamsema ibilisi. Na nani au ibilisi ni nini? (Kiyunani: diabolos). Hebu tuone kama tunaweza kumtambua kutoka katika Biblia.

Katika 1 Yohana 3:8 tumeambiwa kwanini Mungu alimtuma Yesu:

"Kwa makusudi haya Mwana wa Mungu alionekana, ili aziharibu kazi za ibilisi."

Yesu alikuja aziharibu "kazi za ibilisi". Katika Waebrania 2:14 tumeambiwa kwamba Yesu pia alikuja kuziharibu kazi za ibilisi na yeye mwenyewe:

Waebrania 2:14	Maana yake
"Basi kwakuwa watoto wanashiriki damu na mwili,	Waamini (ni watu) Wameumbwa kwa mwili na damu (kawaida ya mwanadamu)
naye pia vilevile alishiriki yayo hayo;	Na Yesu mwenyewe pia kwa njia ileile alikuwa na mwili na damu (kawaida ya mwanadamu)
ili kwa njia ya mauti aweze kuja kumharibu yeye aliye na nguvu za mauti, yaani ibilisi."	Kwa hiyo kwa njia ya kifo chake aliweza kuharibu nguvu za mauti (ambayo ni dhambi) (a ibilisi)

Mstari huu unasema kwamba Yesu alizaliwa kama mtu mwingine yeyote; na hii ilikuwa hivyo ili aweze kumharibu ibilisi, kwa kufa msalabani.

Ikiwa ibilisi alikuwa ni kiumbe anaye pita mwanadamu na ni mwenye nguvu mno, Yesu aliwezaje kumharibu **Kwa kifo chake?** Hii haiwezi kuwa maana ya kweli ya "ibilisi". Angalia Waebrania 2:14 yaisema nguvu ya mauti ni ibilisi nasi tunajuwa kwamba ni **dhambi** inayo tupeleka mautini.

Tutafanya vita siku zote juu ya dhambi?

Kitu kimoja ni yakini: hatutashinda vita katika maisha haya: Wala hatuta fikia muda tunao weza kusema, "Vita dhidi ya dhambi imeisha, na nimeshinda". Kama isingekuwa ni kwa msamaha wa Mungu kwa Yesu Kristo; ambao upo kila siku wa maisha yetu, mashindano yangekuwa hayawezekani. Lakini siku moja mashinaano yataisha!

Wakati Yesu atakapo rudi duniani ili kuuweka Ufalme wa Mungu, wale ambao wamekuwa waaminifu watabadilika - watakuwa sawa na malaika. Watafanywa kutokufa, kama ulivyo jifunza katika Masomo 19, 25 na 27.

Lakini hayo sio yote. Watabadilika hata katika maadili; dhambi haitakuwa na nguvu tena juu yao. Wenye haki hawata taka kufanya mabaya au kufikiria mawazo mabaya. Mashindano yatafikia mwisho na dhambi itakomeshwa milele kutoka kwenye mioyo ya wafuasi. Tunasoma kuhusu hili katika l Wakorintho 15:51-57.

Muhutasari

1. "Ibilisi" ni neno la Biblia la kuitaja dhambi na lazimisho lake katika umbile la mwanadamu.
2. Yesu aliishinda dhambi ndani yake mwenyewe. Kwa sababu hiyo imesemwa kuwa "alimharibu ibilisi".
3. Dhambi ni uovu na haukubaliki kwa Mungu, na wote hufanya dhambi (isipokuwa Yesu).
4. Yatupasa tutubu. Hii maana yake ni kuwa na sikitiko kwa ukweli wa dhambi zetu, na tukiri kuwa tumekosa.
5. Inatubidi tutubu na tuamini kwamba Mungu atatusamehe, hata wakati tukikosa baada ya kuwa wafuasi.

Sura za kusoma: Yakobo 1:12-27; Warumi 6; Warumi 7:14-25
Mistari ya kujifunza: Yakobo 1:14,15

"Bali kila mtu anajaribiwa wakati akivutwa na tamaa zake mwenyewe na kushawishiwa. Basi tamaa ikichukuwa mimba, huzaa dhambi: na dhambi ikitimilika, huleta mauti."

KOZI YA BIBLIA KUTOKA CHRISTADELPHIAN **Na. 31**

UBATIZO

Kusoma: Yohana 3

Wachache wanaojaribu kufanya yalio sahihi wanajikuta wana tatizo kubwa. Moyo wa mwanadamu, Yeremia anatuambia ni "mdanganyifu kuliko vitu vyote nao una ubaya mno" (Yeremia 17:9). Yeyote mnyoofu anayejaribu kuishi maisha mema kuhusu hili litamhuzunisha. Paulo anaeleza kwa ukamilifu jinsi tunavyo ona katika Waraka wake kwa Warumi:

> *"Kwa maana najuwa ndani yangu (yaani ndani ya mwili wangu) halikai jambo jema: maana nia ipo pamoja nami; bali kutenda lililo jema sipati. Kwa kuwa jema nalolipenda kulifanya silitendi; bali lile baya nisilolipenda, ndilo nilitendalo" (Warumi 7:18, 19).*

Hatuwezi kujisaidia weneyewe ... Basi tufanye nini?

Mara tukiisha kuitambua dhambi ndani yetu wenyewe, yatupasa tugeuke na kutengana nayo. Hiyo ndiyo maana ya toba - kugeuka mzima na kisha kwenda njia ya kinyume na dhambi. Hicho ni kitu kingine tusichoweza kufanya pasipo msaada wa Mungu na mafundisho ya Neno Lake. Kwa kifo cha Yesu, tunaweza kuja kwa Mungu na kupata msamaha na kuwa na tumaini la uzima.

Toba huanza wakati tukifahamu jinsi watu wote walivyo ni wenye dhambi na waovu; na – hii ni muhimu - tunapo fahamu hii dhambi na uovu ndani yetu wenyewe

Tunapo tubu katika njia hii, tunakuwa wanafunzi wa Bwana Yesu, tunamfuata na kwenda njia yake. Yesu aliishi maisha makamilifu, na kuwa mfuasi wake maana yake ni kufanya kwa bidii pamoja na uwepo wetu wote kugeuka na kwenda mbali toka kwenye dhambi, na kujaribu kuishi kama alivyo kuwa.

> *"Tuseme nini basi – Tuendelee katika dhambi, ili neema izidi? anakataa. Tutaendeleaje, sisi tulio ifia dhambi, kuishi humo tena?" (Warumi 6:1; 2).*

Hatuwezi kuendelea katika njia zetu wenyewe. Zaidi katika Warumi 6, mtume Paulo anasema:

> *"Dhambi isitawale ndani ya miili yenu ipatikanayo na mauti hata mkazitii tamaa zake. Wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma za dhambi: bali jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kufa, na viungo vyenu kama silaha za haki kwa Mungu."*

Ibilisi aliye haribiwa na Yesu kwa kweli ilikuwa ni dhambi iliyo kuwa ndani yake, kama ilivyo ndani ya kila mtu. (Kumbuka; alirithi umbo tulilo nalo toka kwa mama yake, Mariamu).

Hiki ndicho Waebrania 9:26 inatuambia:

> *" .. yeye (Yesu) alitokea ili aziondoe dhambi kwa dhabihu yake mwenyewe."*

YESU ALIMSHINDA IBILISI
YESU ALIZIONDOA – AU ALISHINDA DHAMBI

Yesu aliishi maisha makamilifu. Yeye "alijaribiwa kwa kila hali kama sisi, hakutenda dhambi" (Waebrania 4:15). Tunajaribiwa, na tunatenda dhambi. Yesu alijaribiwa, lakini kamwe hakutenda dhambi - majaribu kamwe hakuyapa njia. Aliweza kuishinda dhambi kwa njia hii kwa sababu alikuwa ni Mwana wa Mungu.

Alishindana na dhambi maisha yake yote, na mwishowe juu ya msalaba aliiharibu kabisa, kwa kuharibu umbile linaloweza kujaribiwa. Kwa sababu hii, Mungu alimfufua toka wafu, na alimpa "mwili wa utukufu", akawa huru toka majaribu ya kufanya dhambi, naye alipata kutokufa.

Basi ibilisi ni nani?

Dhambi na ibilisi ni kitu kimoja. Yote ambayo Biblia inayasema kuhusu ibilisi, inasema kuhusu dhambi.

Ibilisi ni adui wa Mungu	…. Vivi hivi dhambi
Ibilisi ndiye mjaribu wa mtu	…. Vivi hivi dhambi
Ibilisi ni mdanganyifu	…. Vivi hivi dhambi
Ibilisi anasababisha mauti (Waebr.2:14)	…. Vivyo dhambi hufanya
Ibilisi aliharibiwa na kifo cha Yesu	…. Basi ilikuwa dhambi

Kutoka kwenye milinganisho hii tunaweza kuona kwamba ibilisi na dhambi ni kitu kimoja: Basi, dhambi inatoka wapi?

Biblia inalo jibu la swali hilo, pia. Inatoka ndani ya mioyo yetu wenyewe. Aliwahi kusema Yesu maramoja:

> *"Kutoka ndani ya mioyo ya wanadamu, hutoka mawazo machafu, uasherati, uzinzi, uuaji, wizi; tamaa, ukorofi, hila, ufisadi, matukano, kiburi upumbavu. Haya yote yaliyo maovu yatoka ndani, nayo yamtia mtu unajisi" (Marko 7:21-23).*

Mambo haya mabaya sio tu yamo ndani ya mioyo ya watu wabaya Hata watu walio bora wana mawazo mabaya mioyoni mwao. Mtume Paulo, mtu aliye kuwa mwema, alikuta ni vigumu kutenda mema ,na ni rahisi kufanya mabaya. Anasema katika Warumi 7:18 kwamba ndani ya mwili wake halikai jambo jema: Yakobo anatupa ujumbe uleule. Ni ndani yetu wenyewe, na sio kutoka nje ya nguvu fulani, ambayo inatufanya tuwe na majaribu ya kufanya dhambi. Anasema:

> *"Kila mmoja hujaribiwa wakati akivutwa na tamaa zake mwenyewe, na anashawishiwa. Basi tamaa ikiisha kuchukuwa mimba, inazaa dhambi: na dhambi ikitimilika, huzaa mauti". (Yakobo 1:14-15).*

Ingawa fungu hili la maneno linazungumzia majaribu, haimtaji ibilisi hapa. Kila mmoja hujaribwa na mawazo yake mwenyewe mabaya.

IBILISI NI NGUVU YA DHAMBI INAYO LAZIMISHA NDANI YA MWILI

Ibilisi aliye mjaribu Yesu

Tayari tumeona katika somo la 17, kwamba mjaribu wa Yesu hakuweza kuwa ni ibilisi asiye kufa. Ulimwengu ni mali ya Mungu. Yeye ndiye anayeuongoza, na hakuna kiumbe wa, kupita mwanadamu aliyeweza kutoa "falme zote za ulimwengu" kwa Yesu. Tena, Yesu asinge mfuata tu kiumbe kama huyu, huku akijuwa kwamba na muovu, hadi Yerusalemu au mahali pengine popote!

Kama tulivyo ona, `ibilisi' wa majaribu yake ilikuwa ni mawazo yake mabaya yaliyo kuja moyoni mwa Yesu nia ya kwenda njia zake mwenyewe, badala ya njia ya Mungu, na hivyo kuepuka maumivu ya mateso ya kusulubiwa.

Kwanini 'ibilisi'?

Kwanini imekuwa hivyo Biblia mara nyingi inatumia `neno ibilisi' badala ya kusema tu 'dhambi'? Hapana shaka ili kwamba tuweze kufahamu nguvu za dhambi na udanganyifu wake ulivyo, ndiyo maana ibilisi huyu ameelezewa kama ni kiumbe mwenye nguvu mno.

Yatupasa tuelewe hili kabla ya kuweza kushukuru kabisa jinsi gani sisi sote tunavyo hitaji kuokolewa toka dhambi. Tukifahamu moyoni haja yetu, tunaweza kuanza kushukuru kile Bwana alicho fanya kwa ajili yetu katika kuishinda dhambi.

Ni Mmoja Muumba – Mwenye uweza – wote

Mungu ndiye mkuu. Je, Anaweza kushindana na kiumbe muovu – ibilisi au shetani? Tuna Hawezi.

Lakini shauri lenye nguvu kubwa limekuwa na mataifa yaliyo kabiliana na Mungu nyakati zote. Waajemi wa zamani waliamini kuwa kuna nguvu mbili, ambazo ni kubwa, moja inalingana na Mungu na nyingine inalingana na ibilisi. Yakwanza ilidhaniwa kuwa ni ya kuumba nuru na wema, na yapili ni ya giza na ubaya Jibu la imani hii mbaya, Mungu alipeleka ujumbe kwa kupitia nabii Isaya, kusema

> *"Mimi ni Bwana, wala hapana mwingine, hapana Mungu zaidi yangu mimi: nimekufunga mshipi ijapokuwa hukunijuwa; ili wapate kujuwa toka maawio ya jua, na toka magharibi, ya kuwa hapana zaidi yangu mimi. Mimi ni Bwana, na hapana mwingine zaidi yangu. Nafanya nuru, na kuumba giza: Nafanya amani, na naumba ubaya:* ***Mimi ni Bwana niyatendaye hayo yote****" (Isaya 45:5-7)*

Hapa neno "ubaya" lisichanganyishwe pamoja na "dhambi". Lina maanisha taabu; kama ambazo 'Mungu anawaletea watenda dhambi wasio tii mapenzi yake.)

Ulimwenguni kuna nguvu kubwa moja, inayo panga mambo yote. Huyu ni Muumba mkuu mmoja, anaye vitegemeza vitu vyote kwa neno la uweza Wake. Upinzani kwa **Mungu tu ni kutoka dhambi zilizo ndani ya mioyo ya wanaume na wanawake na maisha yao.**

Dhambi – Tatizo kubwa

> *"Toka mbinguni Bwana aliwachungulia wanadamu, aone kama yuko mwenye akili, amtafutaye Mungu. Wote wamepotoka, wameoza wote pamoja; hakuna atendaye mema, la, hata mmoja" (Zaburi 14:2, 3)*

Ndivyo anavyosema mwandishi wa Zaburi. Paulo katika Warumi 2:23 anatuambia ukweli ule ule anaposema, "Wote wamefanya dhambi, na wamepungukiwa na utukufu wa Mungu." Maneno hayo hayapendezi sana kuyasoma. Hakuna mmoja wetu apendaye kuambiwa "Umekosa!" Tufanyapo makosa, tunajaribu kutoa sababu za, kutaka tuachiliwe, na kumlaumu mwingine. Hatutaki kukutana na ukweli kwamba umbo letu tu wenye dhambi: Hatuwezi kuanza kufahamu ni kiasi gani alicho tutendea Mungu kwa kumtuma Yesu Kristo, wala kuweza kuuitikia upendo Wake, bali mpaka **tufanye** kufahamu hili.

Watu wengi kamwe hawaachi kufikiri kuhusu namna Mungu alivyo wakusudia kuishi maisha yao.